# Kiswahili kama Chombo cha Kutangaza na Kuuza Vyombo vya Habari nchini Kenya

Mark A. Odawo na Jacktone O. Onyango

## Ikisiri

Makala[1] hii inatathmini ufaafu wa matumizi ya maneno ya Kiswahili kama anwani ya vituo vya redio vilivyochipuka katika miaka ya hivi karibuni nchini Kenya. Makala inaangalia jinsi ambavyo hali hii inaweza kuchangia uimarishaji wa lugha ya Kiswahili kwa jumla. Tangu azali na hata enzi ya ukoloni, lugha ya Kiswahili imekuwa zana muhimu ya mawasiliano timilifu sio tu katika ukanda wa Afrika Mashariki bali pia kwa umma mkubwa wa kimataifa. Matumizi ya Kiswahili katika shughuli mbalimbali za binadamu yamekuwa mhimili muhimu wa kukuza na kueneza lugha hii (Tuli, 1985). Katika kizazi cha kisasaleo, harakati za kiuchumi zimejifaragua kutoka biashara ya bidhaa na kujumuisha huduma mbalimbali ikiwemo habari. Kama huduma, habari imekuwa nguzo muhimu ya ufanisi. Dhima ya habari katika maendeleo ya dunia ya kisasaleo imeifanya kuwa huduma ambayo wateja wake wanaongezeka kila uchao. Hii ni hali mojawapo iliyochangia kuchipuka kwa vituo vingi vya redio vinavyoitwa vya Kiswahili ambavyo hutoa matangazo yao kwa Kiswahili. Makala hii inajikita katika kuangalia ufaafu na uamilifu wa majina au anwani na kaulimbiu zenye maneno ya Kiswahili kwa vituo vya redio vilivyoanzishwa na vyombo vya habari katika miaka ya hivi karibuni. Makala inaangalia matumizi ya maneno haya ya Kiswahili kutajia vituo vya redio sawa na mikakati ya kutoa mshawasha kwa wasikilizaji kuonea fahari vituo hivi na kuwateka ili waendelee kuvisikiliza. Kwa namna hii, lugha ya Kiswahili hujitokeza kuwa na uwezo wa kutanguliza, kutambulisha, kutangaza na kuuza vituo hivi kwa umma mkubwa wa wasikilizaji. Kadri wasikilizaji wanavyoendelea kusikiliza na kuchangia mijadala katika vituo hivi ndivyo vituo hivi vinavyoendelea kukubalika kuwa maarufu miongoni mwa wasikilizaji. Vivyo hivyo ndivyo lugha ya Kiswahili inavyoendelea kuimarika, kupanuka na kuenezwa na hivyo kuakisi mustakabali bora wa lugha ya Kiswahili.

## 1.0 Utangulizi

Ijapokuwa kuna nadharia tofauti kuhusu chimbuko na kuenea kwa Kiswahili, wataalam wengi wakiwamo Chiraghdin na Mnyampala (1977) na Chacha (1995) wanaafikiana kuwa lugha hii ina kitovu chake pwani na kuwa ilienea kutoka upwa wa bahari ya Hindi kwenye ukanda wa Afrika Mashariki. Sengo (1995) anadai kuwa Kiswahili ni kizalia cha lugha asili za Waafrika hususan wakazi wa mwambao wa pwani ya Afrika Mashariki kabla ya majilio ya wageni. Kwa mujibu wa Whiteley (1969), Chiraghdin na Mnyampala (1977), Mbaabu (1985, 1991a) na Ogechi (2002), miongoni mwa zana muhimu za kuenea huku kwa lugha tangu awali ni utawala wa kikoloni, siasa, elimu, biashara, ndoa, machapisho na vyombo vya habari ambavyo mchango wake umeongezeka katika miaka ya hivi karibuni kutokana na uwezo wake wa kuwafikia watu wengi kwa wakati mmoja.

[1] Makala hii iliwasilishwa kwa mara ya kwanza katika Kongamano la Kiswahili la CHAKITA lililofanyika katika Taasisi ya Maendeleo ya Mtaala wa Elimu (KICD), Nairobi, Oktoba 23-24, 2014.

Zana hizi zinajitokeza kama sehemu muhimu ya shughuli za binadamu ambazo zimesawiri Kiswahili kama chombo muhimu cha mawasiliano timilifu sio tu katika ukanda wa Afrika Mashariki bali pia kwa umma mkubwa wa kimataifa (Tuli, 1985). Kwa kufanya hivi, lugha hii imefanikisha si mahitaji ya watu binafsi tu bali pia malengo ya makundi na taasisi anuwai. Onyango (2014) anasema kuwa lugha ya Kiswahili inatumiwa kuleta maendeleo ya uchumi nchini Kenya kwa kufanikisha mawasiliano ya kibiashara katika sekta mbalimbali ikiwamo sekta ya huduma za benki. Matumizi ya Kiswahili katika shughuli hizi yamekuwa mhimili muhimu wa makuzi, malezi na maenezi ya lugha hii.

Katika kizazi cha kisasaleo, harakati za kiuchumi zimejifaragua kutoka biashara ya bidhaa na kujumuisha huduma mbalimbali ikiwamo habari. Kama huduma ya habari imekuwa nguzo muhimu ya ufanisi, habari za shughuli za kijamii kama vile sanaa na burudani na zile za kiuchumi kama vile kazi, biashara na uzalishaji huwafikia walengwa wengi kwa haraka zaidi kupitia vyombo vya habari. Hivi ni kusema kuwa dhima ya habari katika maendeleo ya dunia ya kisasaleo imeifanya kuwa huduma ambayo wateja wake wanaongezeka kila uchao.

Hii ni hali mojawapo iliyochangia kuchipuka kwa vituo vingi vya redio vinavyoitwa vya Kiswahili na pia kutangaza kwa lugha ya Kiswahili katika miaka ya hivi karibuni nchini Kenya, hasa baada ya masharti ya utoaji wa leseni ya masafa ya utangazaji kulegezwa mwaka 1999. Maswali tunayojiuliza katika makala hii ni: Je, majina haya ya vituo vya redio yanayosheheni istilahi za Kiswahili yanaathiri vipi usikilizaji wa vituo hivi? Kiswahili kinachotumika kufikisha habari kwa walengwa ni cha kiwango gani? Nini hatima na mustakabali wa lugha ya Kiswahili katika mchakato huu wote? Ni katika kujibu maswali haya ndipo makala hii inatathmini ufaafu wa matumizi ya maneno ya Kiswahili kama anwani na kaulimbiu ya vituo vya redio vilivyochipuka kati ya mwaka 1999 na 2014 na jinsi ambavyo hali hii inaweza kuchangia uimarishaji wa lugha ya Kiswahili kwa jumla. Makala inaangalia matumizi ya maneno ya Kiswahili kutajia vituo vya redio sawa na mikakati ya kutoa mshawasha kwa wasikilizaji kuonea fahari vituo hivi na kuwateka ili waendelee kuvisikiliza. Data za makala hii zilikusanywa kwa kutumia mbinu ya kusikiliza vituo vya redio, mahojiano na wasikilizaji na watangazaji wa vituo vya redio na pia mtandaoni. Makala imegawanywa katika sehemu sita zinazofuatana kama ifuatavyo: utangulizi, vituo vya redio vyenye anwani za Kiswahili, kaulimbiu za vituo vya redio, matumizi ya lugha katika vituo vya redio, mapendekezo na hitimisho.

## 2.0 Vituo vya Redio vyenye Anwani za Kiswahili

Kufikia mwaka 1999, vituo vya redio nchini Kenya vilikuwa 10 pekee. Mwaka 2004 idadi hiyo iliongezeka na kufikia 118 (BuzzKenya.com; Communications Authority of Kenya, 2014). Idadi kubwa ya vituo hivi imeongezeka kuanzia mwaka 2000 wakati sekta ya habari na utangazaji ilipowekwa huru kutokana na masharti ya utoaji wa masafa

ya kutangazia kulegezwa na hivyo kuwaruhusu wamiliki binafsi kuanzisha vituo vya redio.

Mbali na kutoa matangazo yake kwa lugha ya Kiswahili, baadhi ya vituo hivi hutoa matangazo yao kwa lugha ya Kiingereza na lugha nyingine za kiasili. Kati ya vituo 118, vituo 30 vinatumia Kiswahili kama sehemu za anwani za vituo hivyo. Mbinu ya usampulishaji lengwa imetumiwa kuviteua vituo hivyo 30 ambavyo vimetumiwa katika uchanganuzi na maelezo. Vituo hivi ni *Redio Maisha* (Nairobi), *Redio Jambo* (Nairobi), *Baraka FM* (Nairobi), *Redio Salaam* (Mombasa), *Sauti ya Mwananchi FM* (Nakuru), *Rehema FM* (Nairobi), *Redio Pamoja* (Nairobi), *Bahari FM* (Mombasa), *Jambo FM* (Nairobi), *Amani FM* (Nakuru), *Sifa FM* (Voi), *Redio Umoja* (Nairobi), *Redio Kisima* (Nyamira), *Biblia Husema Redio* (Nairobi), *Injili FM* (Kericho), *Mambo FM* (Nairobi), *Pwani FM* (Mombasa), *Imani FM* (Kitale), *Sauti ya Rehema Redio* (*Sayare Radio*) (Eldoret), *Milele FM* (Nairobi), *Pilipili FM* (Mombasa), *Sema Redio* (Kericho), *Redio Simba* (Kampala, Uganda), *Redio Waumini* (Kasarani, Nairobi), *Risala FM* (Garissa), *Bahasha FM* (Nakuru), *Hosana FM* (Nairobi), *Mwangaza FM* (Dodoma, Tanzania), *Neema FM* (Mwanza, Tanzania), na *Rock Mambo FM* (Tororo, Uganda). Baadhi ya vituo vya redio vya Tanzania na Uganda vimejumuishwa katika makala hii kwa sababu matangazo yake hufika pia Kenya.

Mifano michache ifuatayo inaonyesha jinsi majina haya ya Kiswahili yanayotumiwa kutajia vituo vya redio yanavyoafiki na kuathiri usikilizaji wa vituo hivi.

i) *Redio Jambo*

Katika kujinasibisha na wasikilizaji, inazingatiwa kuwa msikilizaji yeyote aliye na jambo linalomkera aliwasilishe katika kituo hiki ili litatuliwe. Kituo hiki huwa na kipindi maarufu kinachoitwa ‘Patanisho’ ambapo wasikilizaji walio na jambo linalotatiza mahusiano yao na wengine wanaruhusiwa kupiga simu ili waweze kupatanishwa kutokana na rai au nasaha za watangazaji pamoja na ushauri wa wasikilizaji wengine wanaoruhusiwa kutoa maoni yao kwa kupiga simu moja kwa moja au kutuma ujumbe mfupi kwa nambari ambayo hutolewa. Aidha, wasikilizaji wanahusishwa katika mijadala ya masuala yanayojiri na kuathiri maisha ya kawaida ya wananchi. Hivyo basi, kituo hiki kimeweza kushawishi wananchi kuwa na ujuzi wa mambo mbalimbali yanayohusu sanaa, michezo, mapenzi na siasa kutegemea usikilizaji wa kituo hiki. Yamkini dhana kama hii inaweza kuhusishwa na vituo kama vile *Jambo FM*, *Mambo FM* na *Rock Mambo FM*.

ii) *Redio Maisha*

Kituo hiki hujaribu kujitambulisha na masuala yanayowakumba wasikilizaji wake katika maisha yao ya kila siku. Kwamba yeyote anayetaka kujua mambo muhimu yanayohusu maisha ya kisasa hana budi kusikiliza kituo hiki. Katika utangazaji wake, kituo hiki kinaangalia maisha kuwa ‘matamu’ na kwamba mada zote zinazofanya maisha kuwa

‘matamu’ kama vile mapenzi, sanaa na michezo hutokana na kusikiliza kituo hiki. Kwa hiyo, wasikilizaji wanakiona kama kitovu cha maisha.

iii) *Milele FM*
Kituo hiki hulenga kuwapasha habari na kuwaburudisha wasikilizaji wake wakati wote au ‘milele’ kama ambavyo jina lake linavyoonesha. Kituo hiki ni maarufu kwa nyimbo za dini ya Kikristo na kilishinda tuzo ya kituo kinachocheza muziki mzuri zaidi wa kidini nchini Kenya kwa miaka mitatu iliyopita. Mtangazaji aliyetambuliwa kuwa bora zaidi ni Eva Mwalili (Groove Awards, 2014). Hivi ni kusema kuwa kituo hiki kinawahakikishia wasikilizaji wake ‘uzima wa milele’.

iv) *Redio Waumini*
Kituo hiki kinajihusisha na matangazo, mijadala na uchezaji wa muziki wenye mada za dini ya Kikristo. Hivi ni kusema kuwa waumini wote wanaweza kutoshelezwa haja zao za kiroho wanaposikiliza kituo hiki. Hivyo basi, kituo hiki kinajitokeza kama chombo cha kuwabadilisha watu ili wawe waumini wa dini ya Kikristo. Hii ndiyo hali ambayo aghalabu hujitokeza katika vituo kama vile *Baraka FM*, *Injili FM*, *Imani FM*, *Rehema FM*, *Sauti ya Rehema Redio* (*Sayare Radio*), *Hosana FM*, *Biblia Husema Redio* na *Neema FM* vinavyolenga kutambulishwa kwa waumini kama vituo vinavyohusishwa na mada za kidini.

v) *Sauti ya Mwananchi FM*
Kituo hiki kinajitokeza kama mtetezi wa mwananchi kwa kuangazia changamoto zinazowakumba. Kinajaribu kuwapa wananchi muda wa kutosha kutoa kauli zao kuhusu masuala yanayowahusu na kuwaathiri moja kwa moja. Maoni ya wananchi yanapewa umuhimu mkubwa na watangazaji wa kituo hiki. Hali inayojitokeza hapa ni kuwa kituo hiki kinajitokeza kama mtetezi wa wasikilizaji (Mahojiano yetu na Wasikilizaji wa Kituo hicho, tarehe10 Oktoba, 2014, Nakuru).

vi) *Redio Umoja*
Kituo hiki hujinasibisha na kuleta umoja, mshikamano na mtagusano miongoni mwa wasikilizaji wake licha ya maoni ya wasikilizaji hao kutofautiana wakati mwingine. Kwa hiyo, kituo hiki hujaribu kujenga fikra za maafikiano na utangamano miongoni mwa wasikilizaji pamoja na watangazaji wa kituo hiki. Kinawasawiri wasikilizaji kama wamoja. Kituo hiki kinaonekana kuwa na mkabala ulio sawa na kituo cha *Redio Pamoja*. Kuna madai kwamba baadhi ya idhaa za redio na wanahabari walichangia katika ghasia zilizofuatia Uchaguzi Mkuu wa mwaka 2007/2008 nchini Kenya maarufu kama *PEV* (Post Election Violence). Inawezekana kwamba kuanzishwa kwa baadhi ya vituo hivi vya redio ni juhudi za wawekezaji kupata faida na pia kuondoa utengano uliopandwa wakati wa ghasia hizo. Kwa hivyo, hizi ni juhudi za kuleta uwiano na utangamano miongoni mwa Wakenya.

vii) *Pwani FM*

Kituo hiki kimsingi kinatoa matangazo yake kutoka maeneo ya pwani, ingawa pia, kinaangazia pia masuala yanayosheheni taifa zima. Hata hivyo, kituo hiki huelekea kuonekana 'miliki' ya wenyeji wa mwambao wa pwani, hasa maeneo ya Mombasa, Kwale na Malindi, ambao ndio hujihusisha nacho zaidi. Hivi ni kusema kuwa wasikilizaji wake wanakionea fahari kubwa kama ilivyo kituo cha *Bahari FM*.

viii) *Redio Kisima*

Kama kisima kinachotoa maji safi kwa matumizi ya binadamu, kituo hiki huwa kama kitovu cha habari zote muhimu anazohitaji msikilizaji kuhusu nyanja zote za maisha. Kituo hiki wakati mwingine huangazia masuala nyeti na mada nzito zinazoamsha hisia na kuwakanganya wasikilizaji kwa nia ya kupata suluhu inayokubalika kwa wote. Mada hizo ni pamoja na ndoa, mapenzi, malezi, lishe na imani. Hii ni kwa sababu kituo hiki kina msingi wake katika dini ya Kiadventista.

ix) *Sema Redio*

Kituo hiki huonekana kutilia mkazo utoaji wa nafasi kwa wasikilizaji wake kusema jambo lolote na kutoa maoni waliyonayo kuhusiana na matukio ya kila siku katika jamii. Mbali na kusemezana wao kwa wao, wasikilizaji husemezana na kujadiliana na watangazaji wa kituo hiki. Hivyo basi, kituo hiki kinaonekana kuthamini maoni na hoja za wasikilizaji wake kuhusu masuala tofauti yanayowashughulisha.

## 3.0 Kaulimbiu za Vituo vya Redio

Baadhi ya vituo vya redio vinavyotumia Kiswahili kama anwani yake pia huwa na kaulimbiu zilizoandikwa kwa lugha hii. Japo baadhi ya vituo vya redio havina majina ya Kiswahili, vimeshehenezwa na kaulimbiu zinazohusisha lugha ya Kiswahili. Hapa inabidi tuvuke mipaka ya redio 30 zilizotajwa katika sehemu ya 2.0 na kutaja mifano ya redio tatu ambazo hutangaza kwa Kiswahili kote nchini na hutumia kaulimbiu za Kiswahili ili kuonyesha jinsi zinavyoathiri usikilizaji. Redio nyingi kati ya zile 30 zilizotajwa hazitangazi kote nchini. Ifuatayo ni baadhi ya mifano na jinsi inavyoathiri usikilizaji wa vituo vya redio husika.

i) *KBC Kiswahili - Redio Taifa*

Kituo hiki kinalenga kutoa habari muhimu zinazogusia masuala ya kitaifa. Hivi ni kusema kuwa kituo hiki kilianzishwa kwa ajili ya taifa zima na kuwa wasikilizaji wote wanaweza kukitumia kutoa sauti au maoni yao kuhusu taifa. Kwa namna hii kituo hiki kinahimiza wasikilizaji kukionea fahari na hivyo kuendeleza fikra za utaifa na uzalendo miongoni mwa wasikilizaji kutokana na kuwashirikisha katika shughuli zinazojenga utangamano.

ii) *Redio Citizen - Chemchemi ya Ukweli*
Jina la kituo hiki inakieleza kuwa kama chanzo na mbubujiko usio na mwisho wa habari za kina na hakika kuhusu nyanja zote za maisha. Ni kana kwamba kituo hiki ndicho kinachopaswa kuaminika kwa usahihi wa habari kwani huenda vingine vimepungukiwa uwezo huo au vinaweza kupotosha ujumbe.

iii) *Redio Maisha - Tuko Mbele Pamoja*
Tamko hili hujaribu kusisitiza umoja na utangamano kati ya watangazaji na wasikilizaji. Ujumbe unaofikishwa hapa ni kuwa umoja na ushirikiano ndio nguzo ya ufanisi. Kwamba kadri kituo hiki kinavyoendelea kujiimarisha ndivyo wasikilizaji pia watakavyoweza kuendelea na kwamba kituo hiki huweza kufifia iwapo wasikilizaji hawapo. Kwa hiyo, kituo hiki kinajaribu kujihusisha na kujinasibisha na wasikilizaji kama vipande visivyoweza kutenganishwa.

iv) *Q FM - Kata Kiu*
*Q FM* (*Kiu FM*) ni kituo kinachojifananisha na kinywaji baridi kinachoweza kunywewa ili kukata kiu ya mnywaji. Hali ya wasikilizaji kutopata habari za kina inaangaliwa sawa na kuwa na kiu. Hivyo basi, yeyote anayetaka kupata taarifa za kweli na burudani za kutosha hana budi kusikiliza matangazo kutoka katika kituo hiki ili 'kukata kiu' yake. Dhana kuu inayotokana na kaulimbiu hii kimsingi huelekea kuoana na ile ya kituo cha *Redio Kisima* inayojulikana kama '*Chota unywe*'.

v) *Milele FM - Wewe ni Wetu*
Ujumbe ulio katika kaulimbiu hii ni ule unaomthamini msikilizaji kama sehemu muhimu ya kituo hiki. Dhana inayojitokeza hapa ni hali ya umoja, mshikamano na utambulisho wa kituo hiki na wasikilizaji wake. Hivi ni kusema kuwa maoni au mchango wa wasikilizaji wa kituo hiki ndiyo yanayojenga msingi wa matangazo ya kituo hiki.

Dhana zinazobainika katika anwani za vituo hivi vya redio na kaulimbiu zake zinaviafiki kwa kuwashawishi wasikilizaji kuendelea kuvisikiliza, kuvionea fahari na kujinasibisha navyo. Kwa njia hii, anwani na kaulimbiu hizi hujitokeza kama mbinu muhimu za kutambulisha na kutangaza vituo hivi kwa wasikilizaji wake.

## 4.0 Matumizi ya Lugha katika Vituo vya Redio

Kwa kuwa idadi kubwa ya matangazo ya vituo hivi vyenye anwani au kaulimbiu zinazotumia maneno ya Kiswahili husikika katika maeneo mengi nchini kwa wakati mmoja, vituo hivi vina nafasi kubwa sio tu katika kueneza lugha hii bali pia katika kuiimarisha na kuikuza kwa umma mkubwa wa wasikilizaji. Kulingana na Marshad (1993:ix), waandishi wa habari wana wajibu mkubwa wa kuikuza na kuipanua lugha hii. Anaendelea kusema kuwa wao ndio wanaotarajiwa kuongeza msamiati, kuivuta lugha hivi na vile wakiinyoosha na kuiwamba kwa nia ya kuiendeleza na kuistawisha. Maoni

haya yanaweza kutolewa pia kuhusu wanahabari wanaotangaza katika vituo vya redio. Kwa hiyo, ni muhimu kutathmini matumizi ya lugha katika vituo hivi. Hii ni kwa sababu uzingativu wa kanuni za matumizi ya lugha hii ni mhimili muhimu wa makuzi na maenezi yake.

Japo watangazaji wa vituo hivi hujizatiti kutumia lugha inayofikia viwango vya sarufi vilivyokubalika, makosa mengi bado yanadhihirika. Mbali na kuonyesha umilisi finyu wa lugha hii na kaida zinazoongoza matumizi yake, baadhi ya watangazaji wameshindwa kutumia lugha yenye mbeko au maadili na istilahi muhimu za lugha hii katika miktadha inayotarajiwa. King'ei (2000) akiwanukuu Senamu na Williams (1991:5) anasema kuwa kiwango cha lugha ya mazungumzo na maandishi kinaendelea kuzorota kila mwaka kutokana na ujuzi duni wa lugha.

Jambo la kusikitisha ni kuwa ukiukaji huu wa kanuni wakati mwingine hufanywa kimakusudi na watangazaji wasiohitimu taaluma hii na hivyo kukosa maadili ya taaluma ya habari na utangazaji (Onyango, 2002:53). Nia ya kuwashirikisha watangazaji hawa huwa ni kuvutia wasikilizaji kutokana na ucheshi na ulumbi wao. Hii ni kwa sababu umiliki wa kibinafsi wa vyombo vya habari kutokana na kuwekwa huru kwa sekta ya habari na utangazaji umeleta ushindani mkubwa baina ya vyombo hivi vya habari kiasi cha kung'ang'ania wasikilizaji. Umiliki huu wa kibinafsi unajitokeza kama uwekezaji wa kibiashara wa vyombo hivi vya habari ambavyo vinatarajiwa kuzalisha faida kuliko vilivyo vyombo vya kupasha habari na vya kukuza lugha hii.

Musau (2001) anasema kuwa hali hii inachangiwa na kukosekana kwa sera dhahiri kuhusu vyombo vya habari nchini Kenya. Hata pale ambapo watangazaji wa baadhi ya vituo wanapojaribu kuzingatia sarufi, ni wakati mwingi ambapo ngeli huvurugwa kiholela licha ya tafsiri sisisi kushehenisha matumizi ya lugha kwenye vituo vingi. Mbaabu (1991) anasema kuwa Kiswahili halisi hakijengwi kwa sarufi pekee. Anataja tafsiri ya neno kwa neno kama kizingiti kikubwa cha ukuaji wa lugha hii. Hii ni kwa sababu tafsiri ya aina hii inaweza kupotosha maana. Baadhi ya kauli zinazotumiwa katika sajili ya mchezo wa kandanda huwa tafsiri sisisi ambazo zinaweza kukanganya na kupotosha maana miongoni mwa wasikilizaji wasiojihusisha mno na sajili hii. Mifano ni kama vile: *dirisha la uhamisho* (*transfer window*) kwa maana ya muda wa kuwasajili wachezaji wapya, *kiatu cha dhahabu* (*golden boot*) kwa maana ya tuzo ya mchezaji anayefunga mabao mengi zaidi katika msimu husika na *muda wa majeruhi* (au muda wa nyongeza) (*injury time/added time*) kwa maana ya muda wa ziada unaoongezwa mchezo unapokaribia kumalizika. Ni muhimu pia kufahamu kwamba lugha ya michezo inatumia misemo/ na nahau zake (taz. Ahmed, 2013).

Vipindi kama 'Maisha Asubuhi' kinachoongozwa na Alex Mwakideu na mchekeshaji Jalang'o (jina kamili Felix Odiwuor) kuanzia saa 12 asubuhi katika kituo cha *Redio Maisha,* 'Milele Breakfast' kinachoongozwa na Ann Waithera na mchekeshaji Mogaka

(Francis Njenga) kuanzia saa 12 asubuhi katika kituo cha *Milele FM* na ‘Jambo Kenya’ kinachoongozwa na Francis Luchivya, Lincoln Njogu na wachekeshaji Inspector Mwala (David Mwambili) na Wilbroda (Jackline Nyaminde) katika kituo cha *Redio Citizen* ni baadhi ya vile visivyomakinikia matumizi sahihi ya lugha. Wanashindwa kuzingatia kauli kuwa ujuzi wa sarufi ndio uti wa mgongo wa matumizi ya lugha (Waihiga, 1999).

Kwa mujibu wa King’ei (2000), matumizi mabaya ya lugha katika vyombo vya habari hasa magazeti hutokana na utohozi wa misamiati ya kigeni, uundaji wa msamiati usiyo sanifu, ujuzi duni wa sarufi na tafsiri mbovu. Baadhi ya watangazaji wa vituo hivi vya redio wakati mwingine wamesikika wakitoa kauli kama “*Ukijibu maswali kumi vizuri tutakupea one hundred K*” badala ya kusema “Ukijibu maswali kumi ipasavyo tutakutuza shilingi elfu mia moja”, “*kama ni mume changu lasima anionyese mapensi na anitimisie maitaji yote*” badala ya “Kama ni mume wangu lazima anionyeshe mapenzi na anitimizie mahitaji yote”, “*Kwaya ya mwiso kutumbuisa kwa serehe ya Masujaa Dei ulikuwa wa Kenyatta University* badala ya “Kwaya ya mwisho kutumbuiza katika sherehe ya siku ya Mashujaa ilikuwa ya Chuo Kikuu cha Kenyatta”, na *Hawa ndio warusa mawe kweli?* badala ya “Hawa ndio wanaorusha mawe kweli.” Huu ni uvurugaji wa lugha.

Changamoto nyingine inayojitokeza katika matumizi haya mabovu ya lugha redioni ni matumizi ya *Sheng*’, yaani uchanganyaji msimbo na matamshi yasiyofaa. Haya hujitokeza sana katika vipindi vya mijadala na muziki. Si ajabu kusikia mtangazaji akitoa kauli kama “*mpenzi wako anakumiss vinoma, mrudie mumeo siste*” (akimaanisha: mpenzi wako anakuhitaji sana, mrudie mumeo dada), “*ukiwa na kitu yoyote ambayo hutumii, enda ukadownload OLX application ili uiuze, usione imezeeka, inaweza kukupatia do poa sana*” (ukiwa na kitu chochote ambacho hutumii, nenda ukakiuze kwenye mtandao wa OLX, usione kimezeeka, kinaweza kukupatia pesa nyingi) na “*manze mzungu wa Gor analazimika kusubstitute mapema baada ya defender kuumia*” (kocha mzungu wa timu ya Gor Mahia analazimika kufanya mabadiliko mapema baada ya mlinzi kuumia) na “*jah man kibao hicho cha Bob Marley kinabamba jo hapa Redio Jambo*” (msikilizaji angalia jinsi muziki huu wa Bob Marley unavyofurahisha sana hapa *Redio Jambo*). Baadhi ya majina ya kutambulisha vipindi fulani katika *Q FM* kama vile ‘Ma afte with Mwafreeka (Makarios Ouma) na Jah Mby’ kinachopeperushwa hewani kuanzia saa 7 mchana na ‘Vuka na Style na Eunice Waithera’ kinachopeperushwa kuanzia saa 12 jioni ni thibitisho la udufu wa matumizi ya lugha katika vituo hivi.

Kutokana na mtindo wa *Sheng*’, Momanyi (2001) anasema kuwa Kiswahili kimefika kwenye njiapanda kwani idadi kubwa ya watu hawawezi kupambanua matumizi bora ya lugha hii. Momanyi (2009) anaendelea kusema kuwa kilugha hiki kinachostahili kuachiwa wanamuziki wa mtindo wa ‘rabsha’, utingo na wauza mihadarati imepenya hadi taasisi za elimu na kuathiri vibaya ufunzaji na matokeo ya somo la Kiswahili. Kulingana na Mbaabu (1991b), ukosefu wa sera dhahiri ya kuendeleza Kiswahili nchini

Kenya ni mojawapo ya sababu zinazochangia kuzuka kwa kilugha cha *Sheng*'. Mbaabu (1995) na King'ei na Musau (2000) wanaafikiana kuwa matatizo ya kimatamshi husababishwa na athari za lugha za kimsingi. Hata hivyo, jambo linalotatanisha ni kuwa watangazaji huhusisha matamshi haya mabovu yanayolingana na yale ya lugha fulani za kiasili ili kuwavutia na kujitambulisha kwa wasikilizaji wanaozungumza lugha hizo.

Hali kadhalika, ni jambo la kawaida kusikia watangazaji wakitumia lugha ya Kiingereza kurejelea istilahi zinazoweza kutafsiriwa kwa urahisi au zilizo na visawe katika lugha ya Kiswahili. Msimbo kama *Thika Highway (*Barabara Kuu ya Thika), *Kenyatta International Conference Centre* (Kituo cha Mikutano cha Kimataifa cha Kenyatta), *Co-Operative House* (Jumba la Ushirika), *Parliament Buildings* (Majengo ya Bunge), *Devolution* (Ugatuzi), *Chief Justice* (Jaji Mkuu), *Court of Appeal* (Mahakama ya Rufaa), *Cabinet Secretary* (Katibu wa Wizara) na *divorce* (talaka) ni maarufu miongoni mwa watangazaji wa vituo hivi vya redio. Hali hii inaelekea kufanya uchanganyaji msimbo kuwa mbinu ya kawaida na maarufu ya mawasiliano katika vituo hivi vya redio. Watangazaji na wanamuziki hutumia *Sheng*' na kuchanganya lugha kwa sababu ya kutaka kuwachekesha wasikilizaji, kujitambulisha kwa wananchi wa kawaida hasa vijana wa mtaani ambao hutumia *Sheng'*, kuwasilisha ujumbe wa siri kwa wana-Sheng' ili kuwatenga wasikilizaji wengine katika mawasiliano na pia kujitambulisha kwa tabaka la wasomi kwa kuchanganya msimbo wa Kiingereza. Sheng' pia husaidia kutangazia bidhaa na huduma zinazowalenga vijana kama vile mipira ya kupanga uzazi.

Kulingana na Mlacha (1995), vyombo vya habari vimekuwa ngazi muhimu katika kusambaza istilahi mpya kwa wananchi kila zinapochipuka. King'ei (2000) naye anasema kuwa vyombo vya habari kama vile redio na runinga vimepiga hatua katika ukuzaji, upanuzi na uendelezaji wa lugha hii kwa kutumia msamiati mpya kuelezea dhana mpya kama vile mtandao. Hali hii imeweza kujitokeza hasa kupitia vipindi maalum vya mafunzo na mijadala vinavyohusisha wataalam wa lugha hii. Hata hivyo, baadhi ya watangazaji wa vituo hivi vya redio vilivyochipuka huendelea kutumia istilahi zilizobuniwa hasa katika uwanja wa teknolojia ya habari na mawasiliano kwa lugha ya Kiingereza. Istilahi kama vile tarakilishi, tovuti, barua-pepe, kipepesi, kiungambali/kisengeretua, mkahawa bwaka, kipakatalishi na rununu ni baadhi ya zile ambazo aghalabu hurejelewa kwa lugha ya Kiingereza.

Ni muhimu kutaja kuwa licha ya udufu huu wa matumizi ya lugha katika vituo hivi vya redio, baadhi yake vimechangia makuzi ya lugha ya Kiswahili kupitia vipindi vinavyoshirikisha maoni na michango ya wanafunzi, walimu, wataalam wa lugha ya Kiswahili wa ngazi ya juu na wakereketwa wengine wa lugha hii. Kwa mfano, katika kituo cha redio cha *KBC Kiswahili*, vipindi ambavyo vimechangia uimarishaji wa Kiswahili ni kama vile 'Lugha Yetu', 'Ongea Lugha Sanifu ya Kiswahili', 'Ukwasi wa Lugha', Chemsha Bongo', na 'Ushikwapo Shikamana'. Hali kadhalika, katika redio ya *Q FM,* kuna kipindi cha 'Kamusi ya Changamka' huku kipindi 'Nuru ya Lugha'

kikipeperushwa katika kituo cha *Redio Maisha.* Aidha, vipindi 'Bahari ya Lugha' na 'Fasihi Fasaha' hupeperushwa katika kituo cha *Redio Citizen*.

## 5.0 Mapendekezo

Ili kuimarisha matumizi ya lugha ya Kiswahili katika vyombo vya habari, serikali inatakiwa ishirikiane na wataalamu pamoja na wadau wengine wa lugha hii katika kuunda sera madhubuti inayohusu matumizi na malezi ya Kiswahili katika vyombo vya habari. Sera husika isiwe maneno tu bali iweze kutekelezwa kikamilifu. Aidha, taasisi inayohusika na utoaji wa leseni ya kuanzishwa kwa vyombo vya habari iweke masharti kuwa watangazaji lazima wawe wamehitimu taaluma ya uanahabari na utangazaji na kwamba vyombo vya habari vinavyokiuka kanuni na maadili haya vipokonywe leseni inayoviruhusu kurusha matangazo.

Ushindani wa kuwateka wateja au wasikilizaji kwa njia inayokiuka matumizi sahihi ya lugha ya Kiswahili uondolewe huku makuzi ya lugha hii yakitiliwa uzito. Hali kadhalika, vipindi vinavyohusisha maoni, michango na mijadala ya wataalamu wa lugha hii viongezwe na kutengewa muda zaidi ili kuelimisha na kutaalamisha umma mkubwa wa wasikilizaji.

## 6.0 Hitimisho

Imebainika wazi kuwa waanzilishi au wamiliki wa vituo hivi wamekuwa makini sana katika uteuzi wa istilahi za Kiswahili za kuitia vituo hivi na kaulimbiu zake. Istilahi zilizotumiwa ni zile zinazowateka wasikilizaji ili kuvionea fahari vituo hivi. Uteuzi huu umefanywa kwa njia inayofanya wasikilizaji kujinasibisha, kujitambulisha na kupendezwa na vituo hivi.

Mbali na kutaka kuwachekesha wasikilizaji na umilisi finyu wa lugha, sababu nyingine inayowafanya baadhi ya watangazaji kutumia lugha kiholela ni ili kuendana na kiwango cha umilisi wa lugha cha wasikilizaji wao. Msukumo mwingine ni hitaji la kukubaliwa na wasikilizaji. Kwa namna hii hata wasikilizaji hawa hujiona kukubalika na kuthaminiwa na watangazaji wanaoonekana kuguswa na hali au changamoto zao. Hatima ya mchakato huu wote ni kuwa vituo hivi hujitokeza kama vyombo vya kueneza lugha hii bila kumakinikia wala kuzingatia viwango vilivyokubalika hasa watangazaji walumbi na wachekeshaji wanapohusishwa.

Msisitizo unaonekana kuwekewa matamko yanayolandana na yale ya lugha nyingine za kiasili ili kutimiza mahitaji ya burudani na mshawasha kwa wasikilizaji, hali inayoweza kusawiri Kiswahili kama lugha yenye mzaha na hivyo kuishushia hadhi. Hivi ni kusema kuwa burudani na utambulisho wa vyombo hivi vya habari kwa wasikilizaji huonekana kupewa uzito kuliko ubora na makuzi ya lugha ya Kiswahili. Kwa hiyo, ijapokuwa vituo hivi hueneza lugha ya Kiswahili kwa kuitumia katika matangazo yao, juhudi za kuikuza na kuilea ni akali. Hivyo basi, lugha hii inajitokeza kuwa na uamilifu mkubwa wa kuvitangaza, kuviuza na kuvikubalisha zaidi kwa umma mkubwa wa wasikilizaji.

## Marejeleo

Ahmed, S. (2013). “Tungo za Kinahau Zinazotoa Taarifa ya Mpira wa Miguu katika Magazeti ya Kiswahili”, *Mulika*. Dar es Salaam: Taasisi ya Taaluma za Kiswahili.

BuzzKenya.com <http://buzzkenya.com/Redio-stations-in-kenya/ 25 Septemba 2016>

Chacha, L. M. (1995). “Chimbuko la Kiswahili”, katika *BARAGUMU, Juzuu la 2 Nam. 1&2* kur. 1-7.

Chiraghdin, S. na Mnyampala, M. (1977). *Historia ya Kiswahili.* Nairobi: Oxford University Press.

Communications Authority of Kenya, June 2014. <http://www.ca.go.ke/ 25 Septemba 2016>

Groove Awards, 2014. <www.grooveawards.co.ke 25 Septemba 2016>

King’ei, K. (2000), “Matatizo ya Matumizi ya Lugha katika Vyombo vya Habari: Mifano kutoka Kenya” katika *Swahili Forum* VII. 45-56.

King’ei, K. na Musau, P. (2000). *Utata wa Kiswahili Sanifu.* Nairobi: Didaxis.

Marshad, H. (1993). *Kiswahili au Kiingereza nchini Kenya?* Nairobi: Jomo Kenyatta Foundation.

Mbaabu, I. (1985). *New Horizons in Kiswahili.* Nairobi: Kenya Literature Bureau.

Mbaabu, I. (1991a). *Historia ya Usanifishaji wa Kiswahili.* Nairobi: Longman Kenya Ltd.

Mbaabu, I. (1991b). “The Impact of Language Policy on the Development of Kiswahili in Kenya, 1930-1990.” Ph.D Thesis, Howard University.

Mbaabu, I. (1995). *Usahihishaji Makosa katika Kiswahili.* Nairobi: Longhorn Publishers.

Mlacha, S.A.K. (mh) (1995). *Kiswahili na Vyombo vya Habari.* Dar-es-Salaam: TUKI.

Momanyi, C. (2001). “Matumizi ya Kiswahili katika Njia Panda: Mtazamo wa Kiisimu-Jamii,” katika *Kiswahili: A Tool for Development – The Multidisciplinary Approach.* Eldoret: Moi University Press.

Momanyi, C. (2009). “The Effect of ‘Sheng’ in the Teaching of Kiswahili in Kenyan Schools,” katika *Journal of Pan African Studies*, 2(8): 127-138.

Musau, P. M. (2001). “Freeing the Airwaves or Cultural Enslavement: The Case of Media in Kenya,” katika *Kiswahili: A Tool for Development – The Multidisciplinary Approach.* Eldoret: Moi University Press. Pp. 36-42.

Ogechi, N. O. (2002). *Mbinu za Mawasiliano kwa Kiswahili*. Nairobi: Moi University Press.

Onyango, J.O. (2002). A*KS 102: Historical Development of Kiswahili*. (Bachelors Module). Institute of Open Learning, Kenyatta University.

Onyango, J. O. (2014). “Kiswahili kama Lugha ya Mawasiliano katika Shughuli za Benki: Changamoto za Tafsiri”. Katika Simala, I., Chacha, L. na Osore, M. (wahr). *Miaka Hamsini ya Kiswahili Nchini Kenya.* Nairobi: Twaweza Communications. 107-112.

Sengo, T. S. Y. (1995). “Hali ya Kutatanisha ya Kiswahili hivi leo Afrika ya Mashariki”, Makala yaliyotolewa katika Kongamano la Nane la Kiswahili, Chuo Kikuu cha Bayreuth, Mei 26-27, 1995.

Tuli, R. S. K. (1985). *Chimbuko la Kiswahili, Kukua na Kuenea kwake Afrika Mashariki.* Arusha: Utalii Exporters and Publications.

Waihiga, G. (1999). *Sarufi Fafanuzi ya Kiswahili.* Nairobi: Longhorn Publishers.

Whitely, W. H. (1969). *Kiswahili: The Rise of a National Language.* London: Methuen.